USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

Jeniffer Peter amepata mtoto wake wa kwanza mwenye afya baada ya mimba kuharibika mara 15 hakuwahi kutumia huduma ya malezi ya kukumbatia mtoto kwa kutumia mtindo wa kangaroo kwa atoto wake wachanga wengine. Alifunzwa kutumia mtindo huu kwa mtoto wake wa 16.

Picha: JHPIEGO

TANZANIA

BORESHA AFYA: LAKE/WESTERN ZONE

Mradi wa USAID Boresha Afya Kanda ya Ziwa na Magharibi unashirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuongeza upatikanaji wa huduma za ubora wa hali ya juu, zilizo kamilifu, na jumuishi kupitia mpango jumuishi wa huduma za afya ya Mama ,uzazi na mtoto, ugonjwa wa malaria kwa mama mjamzito, mtoto mchanga, na huduma za afya za rika balehe. Kwa kufanya haya yote, Boresha Afya inachochea usimamizi wa sera za kitaifa na utashi wa kisiasa ili kuwezesha jamii na kuimarisha utoaji wa huduma za afya. Juhudi hizi zinajengwa kupitia mifumo iliyopo na rasilimali watu ili kuongeza matokeo chanya, ikijumuisha uwekezaji wa awali wa Serikali ya Marekani uliotekelezwa na asasiwashirika wa Boresha Afya.

Yafuatayo ni matokeo tarajiwa ifikapo mwaka 2021:

1. Mazingira bora ya utoaji wa huduma za afya
2. Upatikanaji wa huduma bora, rafiki, na zenye staha zinazozingatia usawa wa kijinsia
3. Ongezeko katika upatikanaji wa huduma bora za afya katika ngazi ya jamii

Yafuatayo ni matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa mradi huu:

1. Kupungua kwa idadi ya vifo na uyevu
2. Utoaji wa huduma jumuishi, mifumo ya usimamizi iliyoboreshwa kikamilifu kwa asilimia themanini (80%) katika wilaya zote zilizoko katika mikoa inayofikiwa na mradi

MATOKEO MPAKA HIVI SASA

- Kuongezeka kwa hudhurio la kwanza ya huduma za mama wajawazito chini ya wiki 12 kutoka asilimia 15 kwa kipindi cha Oktoba - Desemba 2016 hadi kufikia asilimia 39 Oktoba - Desemba 2018 katika mikoa ya Kagera, Mara na Geita.

- Kuongezeka kwa huduma za wajawazito kujifungua kwenye vituo vya afya kutoka wastani wa asilimia 64 mwezi Oktoba - Desemba 2016 hadi asilimia 82 mwezi Oktoba - Desemba 2018 mikoa ya Kagera, Mara na Geita.

- Utendaji ulioboreshwa wa watoa huduma katika huduma jumuishi za magonjwa ya Watoto kwa uwiano (IMCI) katika kurekodi dalili za hatari kutoka asilimia 21 (Oktoba - Desemba 2016) hadi asilimia 58 mwezi Oktoba - Desemba 2018. Utambuzi sahihi pia uliongezeka kutoka asilimia 25 hadi asilimia 40 na matibabu sahihi kutoka asilimia 47 hadi asilimia 60 katika kipindi hicho.

- Kupungua kwa idadi ya visa vya ugonjwa wa malaria vilivyotibiwa bila kuthibitishwa kwa kipimo kutoka asilimia 7.5 (Oktoba - Desemba 2016) hadi asilimia 0.34 mwishoni wa mwaka 2018 katika mikoa yote 7.

- Ongezeko la asilimia 10 katika upimaji wa jumla wa ugonjwa wa malaria kwa wanawake wajawazito wakati wa hudhurio la kwanza la kliniki ya mama mjamzito kutoka asilimia 88 mwezi Oktoba - Desemba 2016 hadi asilimia 98 mwezi Oktoba - Desemba 2018 katika mikoa yote 7.

- Ongezeko kubwa la tiba ya pili ya kujikinga na malaria wakati wa ujauzito (IPTp2) kutoka asilimia 58 mwezi Oktoba-Disemba 2016 hadi asilimia 70 mwezi Oktoba-Disemba 2018 na tiba ya tatu ya kujikinga na malaria wakati wa ujauzito (IPTp3) kuanzia asilimia 20 hadi asilimia 43 katika kipindi kilichotajwa hapo juu katika mikoa yote 7.

- Mnamo mwaka 2018, mradi uliweka rekodi ya ongezeko la asilimia 113 ya huduma za uzazi wa mpango dhidi ya kiwango cha mwaka cha 1,218,070.

BAJETI
Dola za Marekani milioni 59.2

MUDA
Oktoba 2016 – Septemba 2021

Maeneo ya Mradi
Vituo vyote vya afya na jamii katika mikoa saba ya kanda ya ziwa na magharibi (Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Geita, Kigoma, and Simiyu), na msaada katika ngazi ya taifa kwa Tanzania bara na visiwani Zanzibar

MTEKELEZAJI
Jhpiego

MBIA
PATH
EngenderHealth

MAWASILIANO YA USAID
Chonge Kitojo
Afisa Mwakilishi wa Mradi
+ 255 746 700 832
ckitojo@usaid.gov

MAWASILIANO YA MTEKELEZAJI
Dr. Rita Noronha
Mkuu wa Mradi
rita.noronha@Jhpiego.org

KWA TAARIFA ZAIDI
Tovuti: www.usaid.gov/Tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania